

02.04.2026

**TANGAZO LA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA MAFUTA YA DIESEL NA PETROL KWA
MAGARI MAKUBWA NA MADOGO YA KCU (1990) LTD MSIMU 2026/2027**

Zabuni na: KCU/G/2026/2027/01

1. KCU (1990) LTD Inamiliki magari madogo na makubwa ambayo huyatumia katika kazi za kiofisi na shughuli za kuhudumia zao la kahawa katika msimu. Kwa vile magari haya yanatumia nishati ya mafuta ya Diesel na petrol, kituo cha mafuta kitahitajika kutoa huduma hii kwa msimu 2026/2027
2. Maombi yanakaribishwa kutoka kwa wamiliki/waendeshaji wa vituo vya mafuta hapa Bukoba mjini/Manispaa kwa ajili kutoa huduma ya mafuta ya diesel na petroli kwa magari ya KCU (1990) Ltd.
3. Mwombaji sharti aambatishe nakala ya leseni TIN, VAT pamoja na VRN.
4. Mwombaji awe tayari kutoa huduma kulingana na bei elekezi za EWURA.
5. Mwombaji aambatishe nakala ya wasifu wa kampuni.
6. Mwombaji aambatishe nakala ya usajili wa kampuni.
7. Wamiliki/waendeshaji ni lazima wawe wameandikishwa kwa mujibu wa sheria ya makampuni.
8. Mwombaji aambatishe nakala zinaoonesha vielelezo kazi alizowahi kufanya.
9. Ombi la zabuni liwe na jina, anwani halisi ya mwombaji na mahali Ofisi ilipo.
(Physical address)
10. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 200,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955002 General A/C**.
11. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-9 vilivyo tajwa hapo juu.
12. Bhasha ya maombi ifungwe vizuri kwa lakiri na kuandikwa juu yake:- **"MAOMBI YA ZABUNI YA UTOAJI HUDUMA YA MAFUTA YA DIESEL NA PETROL KWA MAGARI YA KCU MSIMU 2026/2027** kwa anwani tajwa hapa chini,
MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBWA.
13. Bhasha hiyo iletwe kwa mkono katika Ofisi ya Manunuzi KCU kabla au mnamo tarehe 20.02.2026 saa 4.00 asubuhi siku ya Jumatatu na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika sherehe ya ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
14. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU

